PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

Toleo Na: 01 Aprili - Juni 2024

# BULLETIN

UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## Karibu tutoe haki katika rufani za zabuni za umma

**Awali ya yote** napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu hadi kufikia hatua hii ya kuanzisha Jarida hili la mtandaoni. Jarida hili ni la kwanza (Aprili – Juni, 2024) kuandaliwa na Mamlaka ya Rufani za Zabuni za Umma (PPAA) na litakuwa linatoka kila baada ya miezi mitatu.

PPAA ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 3 ya Mwaka 2001 ambapo baada ya Sheria hiyo kufutwa, Mamlaka ya Rufani iliendelezwa chini ya Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na kuhuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 baada ya ile Sheria Na. 21 ya Mwaka 2004 nayo kufutwa. Mwaka 2023 Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 nayo ilifutwa na Mamlaka ya Rufani ilihuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya mwaka 2023.

Jarida hili litakuwa likikuletea habari mbalimbali kuhusu utendaji kazi wa PPAA ili kukuwezesha kuyafahamu mafanikio ya PPAA hususan katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Hali kadhalika, kupitia Jarida hili, utafahamu kuhusu Moduli ya kuwasilisha malalamiko/Rufaa kwa njia ya kieletroniki iliyopo katika mfumo wa NeST pamoja na Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024.

Toleo hili ni mwanzo wa matoleo mengine yatakayokuwa yanaandaliwa na PPAA kwa ajili ya kuuhabarisha Umma kuhusu mambo mbalimbali ya PPAA kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa Habari za Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma kwa wadau wake na wananchi kwa ujumla.

Nichukue fursa hii tena kukukaribisha kusoma jarida hili ili uweze kuifahamu vizuri PPAA na shughuli zake mbalimbali.

# Maafisa ununuzi waaswa kutumia mifumo ya ununuzi kieletroniki



*Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande (Mb.) akitoa hutuba yake hivi karibuni wakati akifungua mafunzo ya siku mbili Jijini Dar es Salaam kuhusu moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki*

**Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande (Mb.)** amewaasa maafisa ununuzi wa taasasi za Serikali kuhakikisha kuwa shughuli zote za ununuzi wa umma zinafanyika katika mfumo wa ununuzi wa umma kieletroniki (NeST) ikiwa ni pamoja na kutumia moduli ya kuwasilisha malalamiko kieletroniki.

Agizo hilo limetolewa na Mhe. Chande wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku mbili Jijini Dar es Salaam kuhusu moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA). Mafunzo hayo yalijumuisha Taasisi Nunuzi na wazabuni wa mikoa ya Dar es Salaam, Tanga Morogoro na Pwani.

Pamoja na mambo mengine, Mhe. Chande amezielekeza Taasisi zote za serikaali kutumia mfumo wa ununuzi kieletroniki bila kuwa na kisingizio chochote kile.



Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande (Mb.) akizungumza na washiriki wa mafunzo siku mbili Jijini Dar es Salaam kuhusu moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki

"Napenda kuzielekeza taasisi nunuzi zote nchini kuhakikisha wanatumia mfumo wa NeST na endapo yatatokea malalamiko basi mshikamane kwa pamoja kati ya mlalamikaji, mtoa haki na mlalamikiwa na kuhakikisha haki inapatikana," alisema Chande.

Kadhalika, Mhe. Chande amewaelekeza wazabuni kuhakikisha kuwa wanazingatia taratibu za ununuzi wa umma kwa umakini na endapo kunakuwa na ukiukwaji wa taratibu za ununuzi katika michakato husika, wahakikishe malalamiko au rufaa zinazotokana na ukiukwaji wa taratibu hizo, zinawasilishwa kwa kuzingatia muda ulioainishwa kwenye sheria.

"PPAA kwa kushirikiana na PPRA hakikisheni kuwa mnatoa uelewa/mafunzo ya kutosha kuhusu Moduli hii mpya ya kupokea na kushughulikia malalamiko ya wazabuni kwa njia ya kielektroniki ili kuisaidia Serikali kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika katika miradi mbalimbali," ameongeza Mhe. Chande.

Aidha, Waziri Chande ameielekeza PPAA kuhakikisha kuwa inashirikiana na PSPTB katika maamuzi wanayotoa ili PSPTB iweze kuwachukulia hatua stahiki wataalamu wa ununuzi na ugavi pindi wanapokiuka maadili ya taaluma yao.

Awali Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando alisema kuwa Mamlaka ya Rufani iliundwa ili kutatua migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa umma kwa muda mfupi zaidi tofauti na Mahakama za kawaida ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli, huduma na miradi ya Serikali kwa wakati. "Sambamba na hilo kupitia malalamiko na rufaa zinazoshughulikiwa, Mamlaka ya Rufani inaisaidia Serikali kwa kuhakikisha Sheria ya Ununuzi wa Umma inazingatiwa ili kupata thamani halisi ya fedha zake kupitia ununuzi," alisema Bw. Sando

Bw. Sando ameongeza kuwa Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mamlaka ya Rufani imeendelea kutekeleza jukumu lake kuu la utatuzi wa migogoro itokanayo na michakato ya Ununuzi wa Umma kwa haki, uwazi, uadilifu na kwa muda mfupi ili kuwezesha upatikanaji wa huduma bora na kwa wakati kwa wananchi. Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu, Mamlaka ya Rufani imefanikiwa katika maeneo ya falsafa ya R nne (4R) za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando ameongeza kuwa muda wa ushughulikiaji malalamiko au rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma umepungua kutoka siku saba (7) hadi siku tano (5) za kazi.

Kadhalika, muda wa Afisa Masuuli kushughulikia malalamiko ya zabuni kutoka siku saba (7) za kazi hadi siku tano (5) za kazi na pale ambapo Afisa Masuuli ataunda jopo la mapitio ya malalamiko basi atakuwa na siku saba (7) za kazi na atatakiwa kuwajulisha washiriki wote wa zabuni hiyo kuundwa kwa jopo; na muda wa Mamlaka ya Rufani kushughulikia malalamiko au rufaa umepunguzwa kutoka siku arobaini na tano (45) hadi siku arobaini (40) ■


BULLETIN
Maafisa ununuzi waaswa kutumia mifumo ya ununuzi kieletroniki

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
James Sando

**Mhariri**
Florida Mapunda

**Wajumbe**
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga
Violet Limilabo

**Katibu**
Nelson Kessy

**Mawasiliano:**
**Katibu Mtendaji**
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz

# Wadau wa ununuzi washauriwa kuzingatia uadilifu, uaminifu na haki



*Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Moses Dulle akiwasilisha hutuba wakati wa kufunga mafunzo ya siku mbili juu ya moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki hivi karibuni Jijini Dar es Salaam*

**Serikali imewapa changamoto wadau wa Sekta ya ununuzi wa umma** kuhakikisha wanazingagtia misingi ya uadilifu, uaminifu na haki katika michakato ya ununuzi wa umma ili kuiwezesha Serikali kupata thamani ya fedha.

Rai hiyo imetolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba katika hotuba yake iliyosomwa na Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Moses Dulle wakati wa kufunga mafunzo ya siku mbili juu ya moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa taasisi nunuzi na wazabuni wa mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Pwani, Jijini Dar es Salaam.

Dkt. Mwamba amesema umuhimu wa mafunzo kuhusu moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki umechagizwa na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoendelea duniani hususan kutungwa upya kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 na kuruhusu hatua za mageuzi kuchukuliwa.

"Kutungwa upya kwa sheria ya ununuzi wa umma 2023 kumesaidia kuongeza ufanisi, haki, uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma," alisema Dkt. Mwamba

Hotuba yake imeongeza kuwa asilimia 70 ya matumizi ya Serikali huelekezwa katika ununuzi wa umma ambapo kwa kutumia mfumo mpya, uwazi na uwajibikaji utaisaidia serikali kupata thamani halisi ya fedha katika miradi yake.

Pamoja na mambo mengine, Katibu Mkuu ameielekeza PPAA kuendelea kutoa uelewa wa moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki kwa wadau wa ununuzi na kujenga uelewa wa pamoja.

Awali, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Mhe. Jaji Mstaafu Sauda Mjasiri amesema kuwa mafunzo hayo yatakuwa endelevu ili kuwawezesha wadau wa sekta ya ununuzi nchini kuwa na uelewa wa pamoja.

"Kupitia mafunzo haya ya siku mbili mada mbalimbali zimewasilishwa hususan moduli ya uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko au rufaa..........kutokana na mwitikio ulioonekana umeonesha nia njema ya kuwafikia wadau wengi na kuongeza uelewa na ufanisi katika sekta ya ununuzi nchini," alisema Jaji Msafiri.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando alisema kuwa Mamlaka ya Rufani itaendelea kushirikiana na PPRA kusimamia zoezi la kutoa mafunzo ya mfumo mpya wa kuwasilisha na kushughulikia malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki (Complaint and Appeal Management) ili kuwawezesha wadau wengine kujua jinsi ya kutumia moduli hii ya malalamiko.

Bw. Sando aliongeza kuwa PPAA itaendelea kuzielimisha taasisi nunuzi na wazabuni wa kanda nyingie kuhusu mfumo huu mpya husussan Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko/rufaa kieletroniki.

Mafunzo hayo yaliyoanza tarehe 29 – 30 Mei, 2024 yalitolewa kwa taasisi nunuzi, wazabuni pamoja na mawakili yamelenga kuwajengea wadau hao uelewa kuhusu mfumo mpya wa kuwasilisha na kushughulikia malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki (Complaint and Appeal Management) ili kuwawezesha wadau wengine kujua jinsi ya kutumia moduli hiyo ya malalamiko ■



*Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Mhe. Sauda Mjasiri akizungumza na washiriki wakati wa kufunga mafunzo ya siku mbili juu ya moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki hivi karibuni Jijini Dar es Salaam*

# PPAA mbioni kukamilisha Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akihutubia wazabuni na wanasheria wakati wa kutoa maoni ya Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 hivi karibuni Jijini Dar es Salaam*

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** ipo katika hatua za mwishoni za kupokea maoni ya Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 ili kuiwezesha Sheria ya Ununuzi Umma ya Mwaka 2023 kutekelezeka kwa ufanisi, ambapo pamoja na mambo mengine, Kanuni hizi zitatoa wigo mpana wa kuwasilisha malalamiko na rufaa.

Akiongea katika kikao kazi cha kupokea maoni ya wazabuni na wanasheria Jijini Dar es Salaam, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende amewataka wazabuni kutoa maoni chanya ambayo yataiwezesha PPAA kupata Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 zinazoendana na wakati na zitakazoiwezesha Serikali kupata thamani halisi ya fedha katika sekta ya ununuzi wa Umma.

“Kwa kuwa sheria mpya ya ununuzi wa umma ya Mwaka 2023, imeelekeza shughuli zote za ununuzi wa Umma kufanyika Kieletroniki kupitia mfumo wa NeST, na kwa kuwa moduli mpya ya kupokea na kushughulikia malalamiko au rufaa zitokanazo na michakato ya Ununuzi wa Umma imekamilika, wazabuni mjitahidi kutoa maoni yatakayowasaidia kuepukana na malamiko au rufaa zisizo na ulazima kwani kufanya hivyo kutaokoa muda na kusaidia Serikali kupata thamani halisi ya fedha,” amesema Dkt. Luhende.

Pamoja na mambo mengine, Dkt. Luhende ameongeza kuwa Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 imeboresha masuala mbalimbali ikiwepo kupunguzwa kwa muda wa kushughulikia malalamiko na rufaa zinazotokana na



*Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga akiwaeleza wazabuni na wanasheria juu ya mabadiliko ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya 2023 wakati wa kutoa maoni ya Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 hivi karibuni Jijini Dar es Salaam*




*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akieleza jinsi PPAA ilivyo jipanga kukamilisha Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 hivi karibuni Jijini Dar es Salaam*

michakato ya Ununuzi wa Umma.

"Muda wa siku saba za kazi kwa ajili ya kusubiri malalamiko ya wazabuni kabla ya kutoa tuzo umepunguzwa na kuwa siku tano za kazi.............sambamba na hilo muda wa PPAA kushughulikia malalamiko au rufaa umepunguzwa kutoka siku arobaini na tano hadi siku arobaini," ameongeza Dkt. Luhende.

Kwa upande wake, Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Wizara ya Fedha, Dkt. Frederick Mwakibinga amesema mabadiliko ya Sheria ya Ununuzi wa Umma yamekuwa yakifanyika mara kwa mara kwa lengo la kupunguza muda, kuongeza uwazi na usawa katika shughuli za ununuzi wa umma, kuongeza ushindani na kupunguza mianya ya rushwa.


"Sote tumesikia kuwa muda wa kushughulikia malalamiko na rufaa umepunguzwa na shughuli zote za ununuzi wa Umma zinafanyika kwa njia Kieletroniki na PPAA ipo katika mchakato wa kukamilisha Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 ambapo baada ya kukamilika zitasaidia kuboresha Sekta ya Ununuzi wa umma," alisema Dkt. Mwakibinga.

Naye Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) Bw. James Sando amesema zoezi la kupokea maoni kuhusu Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma ni mwendelezo wa kuwashirikisha wadau wote wanaohusika na sekta ya ununuzi. "Kanuni hizi zinaandaliwa ili kuifanya Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma 2023 kutekelezwa kwa ufanisi na kuiwezesha Serikali kupata thamani halisi ya fedha," alisema Bw. Sando

Katika kikao hicho, Wakili wa kujitegemea, Bw. James Kasusura aliipongeza PPAA kwa kazi nzuri ya kusimamia mabadiliko ya Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma ikiwa ni pamoja na muda wa kutoa maamuzi katika mashauri yanayowasilishwa katika Mamlaka hiyo.




*Mzabuni Bi. Eva Tunduru akitoa maoni kuhusu Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 hivi karibuni Jijini Dar es Salaam*




*Wakili wa kujitegemea, Bw. James Kasusura akitoa salamu za pongezi kwa niaba ya mawakili wa kujitegemea baada ya kumaliza mafunzo ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko/rufaa kieletroniki*

"Tunategemea kuboresha muda, kuongeza zaidi uwazi katika *tendering*, na uwazi katika mfumo na watu wavione na kuvitekeleza," alisema Bw. Kasusura

Mwaka 2004, Serikali iliifuta Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 3 ya Mwaka 2001 kutokana na upungufu uliokuwepo katika Sheria hiyo na kutunga Sheria Na. 21 ya mwaka 2004 ambayo ilitumika hadi mwaka 2011. Aidha, Serikali iliifuta Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.10 ya Mwaka 2023 ili kukidhi mahitaji ya sasa ambayo yalishindwa kutekelezwa na Sheria ile ya 2011 ■

# Miaka Mitatu ya Rais Samia: PPAA yaimarisha utoaji haki, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika zabuni za umma



**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 3 ya Mwaka 2001 ambapo baada ya Sheria hiyo kufutwa, Mamlaka ya Rufani iliendelezwa chini ya Sheria ya Ununuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na kuhuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 baada ya ile Sheria Na. 21 ya Mwaka 2004 nayo kufutwa. Mwaka 2023 Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 nayo ilifutwa na Mamlaka ya Rufani ilihuishwa tena kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya mwaka 2023.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, jukumu kuu la PPAA ni kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya malalamiko au rufaa zitokanazo na maamuzi ya Maafisa Masuuli wa Taasisi mbalimbali za Umma katika michakato ya ununuzi wa Umma. Pia, ina jukumu la kupokea na kusikiliza malalamiko ya wazabuni ambao hawakuridhishwa na uamuzi wa kufungiwa (blacklist) na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

PPAA ni chombo mbadala cha kutatua migogoro itokanayo na michakato ya ununuzi wa umma kwa muda mfupi zaidi tofauti na Mahakama za kawaida ili kuwezesha shughuli, huduma na miradi ya Serikali pamoja na kuhakikisha Sheria ya Ununuzi wa Umma inazingatiwa ili kupata thamani ya fedha.

**129**

Jumla ya mashauri ambayo PPAA imeweza kushughulikia ambayo yaliyotakana na michakato ya Ununuzi wa Umma kwa kipindi cha miaka mitatu.

**27**

Jumla ya tuzo ambazo PPAA ilizuia kutolewa kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitalaamu za kutekeleza miradi

Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi Imara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kudumisha, misingi ya utawala bora ikiwemo haki na usawa, pamoja na kuendelea kusimamia miradi ya kimkakati yenye tija kwa nchi na hivyo kuiwezesha Serikali kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa Umma.

Kwa kuwa takribani asilimia 70 ya Bajeti ya Serikali hutumika kwa ajili ya Ununuzi wa Umma. Hivyo, Sheria, Kanuni na Miongozo ya Ununuzi wa Umma zinaiwezesha Serikali kuendelea kuimarisha sekta ya Ununuzi wa umma.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, PPAA imeendelea kutekeleza jukumu lake kuu la utatuzi wa migogoro itokanayo na michakato ya Ununuzi wa Umma kwa haki, uwazi, uadilifu na kwa muda mfupi na kufikia malengo ya kutoa huduma bora na kwa wakati kwa wananchi.

**Katika kipindi cha miaka mitatu, PPAA imefanikiwa katika maeneo ya falsafa ya R nne (4R) za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kama ifuatavyo:-**

**i. Usuluhishi wa Migogoro (Reconciliation)**

PPAA imeweza kushughulikia jumla ya mashauri 129 yaliyotakana na michakato ya Ununuzi wa Umma. Kudhibiti utoaji wa tuzo kwa wazabuni



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akizungumza na washiriki wakati wa kufungua mafunzo ya siku mbili juu ya moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/ rufaa kwa njia ya kieletroniki hivi karibuni Jijini Dar es Salaam*

# Miaka mitatu ya Rais Samia

ambao walipendekezwa kupata zabuni bila kuwa na sifa stahiki. PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa wazabuni 27 wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika. Hatua hii iliepusha utekelezaji usioridhisha wa miradi unaosababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi. Hili litawezekana kwa kujenga jamii inayopata haki sawa mbele ya sheria, isiyobagua na inayotoa fursa sawa za kiuchumi.

Serikali ya awamu ya Sita chini ya Rais Samia inaamini kuwa usuluhishi wa migogoro hauwezi kupatikana penye ubaguzi na pale ambapo kuna wanaokosa fursa na haki zao za kiuchumi na kiraia. Hivyo PPAA kuzuia utoaji wa tuzo kwa wazabuni 27 waliokosa sifa inaweka uzito katika usuluhishi wa migogoro ambayo ni moja kati ya falsafa za Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

PPAA imeendelea pia kudhibiti taasisi nunuzi kukiuka taratibu za kisheria hasa katika kufanya tathmini ya zabuni (tender evaluation); katika baadhi ya mashauri, PPAA ilifanikiwa kubaini ukiukwaji wa taratibu za kufanya tathimini na taasisi nunuzi ikiwemo kutokuzingatia vigezo vilivyowekwa katika kabrasha la zabuni au kuongeza vigezo vipya ambavyo havikuwepo awali.

Kwa kufanya hivyo, PPAA ilihakikisha kuwa zabuni zinatolewa kwa wazabuni wenye sifa na wanaotoa huduma zenye ubora, hivyo kuiwezesha Serikali kupata thamani halisi ya fedha na kuepusha upotevu wa fedha za serikali katika michakato ya ununuzi wa umma.



**R4**

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

- **Usuluhishi**
- **Mageuzi**
- **Kujenga Upya**
- **Ustahimilivu**

**ii. Mageuzi (Reform)**

Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha kutungwa upya kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 na kuruhusu hatua za mageuzi kuchukuliwa pale ambapo ilibainika kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu katika mchakato wa ununuzi. Kupitia Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma mageuzi mbalimbali yalifanyika yakiwemo:-

**a)** Kupunguza muda wa ushughulikiaji malalamiko au rufaa zinazotokana na michakato ya Ununuzi wa Umma. Mfano, muda wa siku saba (7) za kazi kwa ajili ya kusubiri malalamiko ya wazabuni (cool off period) kabla ya kutoa tuzo umepunguzwa na kuwa siku tano (5) za kazi. Muda huo hautajumuisha njia za ununuzi ambazo hazihitaji ushindani ambazo ni *single source, minor value procurement* na *shopping;* muda wa Afisa Masuuli kushughulikia malalamiko ya zabuni kutoka siku saba (7) za kazi hadi siku tano (5) za kazi na pale ambapo Afisa Masuuli



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akizungumza na washiriki wakati wa kufunga mafunzo ya siku mbili juu ya moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki hivi karibuni Jijini Dar es Salaam*

# Miaka mitatu ya Rais Samia



ataunda jopo la mapitio malalamiko basi atakuwa na siku saba (7) za kazi za kushughulikia na atatakiwa kuwajulisha washiriki wa zabuni kuwepo kwa jopo; na muda wa PPAA kushughulikia malalamiko au rufaa kutoka siku arobaini na tano (45) hadi siku arobaini (40).

**b)** Kuweka masharti ya lazima kwa taasisi nunuzi kufanya ununuzi kupitia mfumo wa kieletroniki. PPAA imefanikiwa kuanzisha moduli mpya ya kuwasilisha rufaa/malalamiko kwa njia ya kieletroniki (e-complaints). Moduli hiyo inarahisisha uwasilishaji wa malalamiko na kutoa fursa kwa wazabuni wengi zaidi kuwasilisha malalamiko yao. Aidha, moduli hiyo ni rafiki na inaokoa muda wa kuwasilisha malalamiko. Moduli ya e-complaints imewekwa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kieletroniki (NeST), uliojengwa chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Kwa kuwezesha moduli ya kuwasilisha malalamiko kieletroniki (e-complaints) kwenye Mfumo wa NeST, PPAA itaweza kufanya mapitio ya mchakato mzima wa zabuni inayolalamikiwa, hivyo kuwezesha kupata uhalisia zaidi na kutoa uamuzi kwa haraka, kwa haki na usawa.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia, PPAA pia imefanikiwa kuboresha kanuni za rufaa za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024 ambapo pamoja na mambo mengine, Kanuni hizo zimetoa wigo mpana wa kuwasilisha malalamiko ikijumuisha mfumo mzima wa ununuzi wa umma (supply Chain system). Mabadiliko katika sheria ya ununuzi yataleta ushindani wa haki na kuwapa wazabuni fursa ya kushindana kwa haki na uwazi katika zabuni mbalimbali.

**115**

Idadi ya mashauri kati ya **117** ambayo PPAA imeshughulikia hadi kufikia Mwezi Machi, 2024.



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akielezea mafanikio ya PPAA kwa kipindi cha miaka mitatu chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan*

**iii. Kujenga upya (rebuild)**

Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha na kuboresha usimamizi wa sekta ya ununuzi wa umma nchini, hatua ambayo imeiwezesha PPAA kuwajengea uwezo Wajumbe wa Mamlaka na Watumishi wake na kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia vifaa muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya PPAA na kuiwezesha Serikali kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa wakati na kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa Umma.

Hadi kufikia Machi, 2024 PPAA ilikuwa imeshughulikia mashauri 115 kati ya mashauri 117 yaliyowasilishwa. Aidha, asilimia 23 ya mashauri hayo yalibainika kuwa na kasoro mbalimbali katika mchakato wake wa ununuzi. Endapo mashauri hayo yasingeshughulikiwa na mchakato wa ununuzi ukaendelea Serikali ingeweza kupoteza kiasi cha shilingi TZS. 543,038,763,639 kwa kuwapa tuzo wazabuni wasiokuwa na sifa za kutekeleza miradi ya maendeleo.

**iv. Ustahimilivu (Resilience)**

Licha ya changamoto za kiuchumi zinazoendelea kuikabili dunia na kutikisa uchumi kama vile Covid 19, vita ya Urusi na Ukraine pamoja na kuadimika kwa fedha za kigeni (USD), bado Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuiwezesha PPAA kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Serikali imeendelea kutoa fedha kwa wajumbe wa Mamlaka ya Rufani na watumishi na kuwezesha utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi na wakati. Katika kipindi cha miaka mitatu, PPAA imeweza kushughulikia jumla ya mashauri 129 yaliyotakana na michakato ya Ununuzi wa Umma ■

# Kanuni za Ununuzi wa Umma za Uwasilishaji wa Rufaa za Mwaka 2024 Mbioni Kuanza



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akifafanua jambo kwa wakuu na wawakilishi wa taaasisi zinazosimamia Ununuzi wa Umma Serikalini waliposhiriki kujadili mapendekezo ya Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 katika ukumbi wa PPAA Jijini Dodoma*



*Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga akieleza jambo katika kikao cha Wakuu wa taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi Serikalini walipokutana Dodoma kujadili mapendekezo ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Uwasilishaji wa Rufaa za Zabuni za Umma za Mwaka 2024*



*Naibu Katibu Mtendaji wa PPAA, Bi. Florida Mapunda akifafanua jambo wakati wa kikao cha Wakuu wa taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi Serikalini walipokutana Dodoma kujadili mapendekezo ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Uwasilishaji wa Rufaa za Zabuni za Umma za Mwaka 2024*

**Wakuu wa Taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi Serikalini** wamekutana katika kikao cha siku moja na kujadili mapendekezo ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Uwasilishaji wa Rufaa za Zabuni za Umma za Mwaka 2024.

Akiongea katika kikao hicho kilichofanyika Mwezi Aprili 2024 Jijini Dodoma Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga pamoja na mambo mengine, aliielekeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kuhakikisha kuwa inaboresha kanuni hizo kama ilivyoelekezwa na wajumbe wa kikao na kuiweza Serikali kupata thamani halisi ya fedha.

"Maboresho ya kanuni hizi ni muhimu sana kwa ustawi wa sekta ya Ununuzi na uchumi wa Taifa letu kwa ujumla hivyo ni vyema tukaboresha maoni yote yaliyotolewa na wadau hapa......lakini pia tuzingatie na kuhakikisha kuwa maboresho haya yanaakisi mfumo mzima wa ununuzi (supply chain)," alisema Dkt. Mwakibinga.

Kwa Upande wake katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando aliwashukuru wajumbe walioshiriki na kutoa maoni yao kuhusu maboresho ya kanuni hizo na kuwahakikishia utekelezaji wa haraka katika maeneo yaliyopendekezwa kuboreshwa.

"Mwenyekiti na wajumbe mlioshiriki kikao cha leo, naomba kuwahakikishia kuwa mapendekezo yote mliyoyatoa hapa leo tumeyapokea na tutayafanyia kazi haraka iwezekanavyo ili kuboresha sekta ya ununu na uchumi wa Taifa kwa ujumla" alisema Bw. Sando

Moja ya maboresho katika kanuni hizo ni pamoja na masharti ya lazima kwa taasisi nunuzi kufanya ununuzi kupitia mfumo wa kieletroniki (NeST). PPAA imefanikiwa kuanzisha moduli ya kupokea na kushughulikia rufaa/malalamiko kwa njia ya kieletroniki (e-complaints). Moduli hiyo inarahisisha uwasilishaji wa malalamiko kwa wazabuni wengi zaidi kuwasilisha malalamiko yao. Aidha, moduli hiyo ni rafiki na inaokoa muda wa kuwasilisha malalamiko. Moduli ya e-complaints imewekwa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kieletroniki (NeST), uliojengwa chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Wakuu wa Taasisi zilizoshiriki katika kikao hicho ni Afisa Mtendaji Mkuu Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalin (GPSA) Prof. Geraldine Rasheli, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Ununzi na Ugavi (PSPTB), Bw. Godfred Mbanyi, Mwakilishi kutoka Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma (PPRA) pamoja na wajumbe wengine kutoka Wizara ya Fedha ■

# PPAA mguu sawa kutumia Kanuni za Rufaa za 2024 mwezi Julai 2024




*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akiongea na washiriki wa kikao kazi cha kupokea maoni ya uandaaji wa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 hivi karibuni Jijini Dodoma. Kanuni hizo zitasaidia kuiwezesha Sheria ya Ununuzi Umma ya Mwaka 2023 kutekelezeka kwa ufanisi.*

**SERIKALI kupitia Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA)** imejipanga kuanza kutumia rasmi Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024 kuanzia mwezi Julai 01, 2024.

Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amebainisha hayo Jijini Dodoma wakati wa kikao kazi cha kupokea maoni ya uandaaji wa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 ili kuiwezesha Sheria ya Ununuzi Umma ya Mwaka 2023 kutekelezeka

Kadhalika, Bw. Sando aliongeza kuwa Sheria Na.10 ya Ununuzi wa Umma ilitungwa na kupitishwa na Bunge mwezi Septemba 2023 ambapo ili iweze kutumika kwa ufanisi inategemea Kanuni za Ununuzi wa Umma ambazo zipo katika hatua mbalimbali na zitakamilika na kuanza kutumika rasmi katika mwaka ujao wa fedha.

"Sheria ipo tayari lakini haiwezi kutumika bila kuwa na kanuni ndio mana tuko hapa kwa ajili ya kupokea maoni ya wadau wa ununuzi kuhusu Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 ili kuiwezesha Sheria ya Ununuzi Umma ya Mwaka 2023 kutekelezeka kwa ufanisi,"alisema Sando.

Awali Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, kutoka Wizara ya Fedha, Dkt. Frederick Mwakibinga ambaye alimwakilisha Mgeni Rasmi - Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo alisema Serikali imefanya maboresho makubwa katika Sheria hizo, hivyo watu watarajie mageuzi makubwa.

Dkt. Mwakibinga alisema baada ya Kanuni kukamilika zitasaidia wananchi hususani wazabuni na wadau wa ununuzi kwenda kutumia kanuni ambazo zimekamilika na kuboreshwa na kuisaidia Serikali kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa Umma.

Alifafanua zaidi kuhusu mabadiliko ya Sheria ambapo amesema Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 imeboresha masuala mbalimbali ikiwepo kupunguzwa kwa muda wa kushughulikia malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya Ununuzi wa Umma.

"Mfano, muda wa siku saba (7) za kazi kwa ajili ya kusubiri malalamiko ya wazabuni (cool off period) kabla ya kutoa tuzo umepunguzwa na kuwa siku tano (5) za kazi. Muda huo hautajumuisha njia za ununuzi ambazo hazihitaji ushindani kama vile *single source, minor value procurement* na *shopping*, kadhalika muda wa Afisa Masuuli kushughulikia malalamiko ya zabuni umepunguzwa kutoka siku saba (7) za kazi hadi siku tano (5) za kazi pale ambapo hataunda jopo,"alisema Dkt. Mwakibinga

Aidha, Dkt. Mwakibinga aliongeza kuwa kutokana na maboresho hayo endapo Afisa Masuuli ataunda jopo la mapitio ya malalamiko basi atakuwa na siku saba (7) za kazi na atatakiwa kuwajulisha washiriki wote wa zabuni juu ya uundwaji wa jopo hilo. Sambamba na hilo muda wa PPAA kushughulikia malalamiko au rufaa umepunguzwa kutoka siku arobaini na tano (45) hadi siku arobaini (40).

"Hivyo ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, PPAA ipo katika mchakato wa kuandaa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024 ambapo pamoja na mambo mengine, Kanuni hizo zitatoa wigo mpana wa kuwasilisha malalamiko. Mabadiliko hayo yatawapa wazabuni fursa ya kushindana kwa haki na uwazi katika zabuni mbalimbali," aliongeza Dkt. Mwakibinga ■



*Sehemu ya washiriki wa kikao kazi cha kupokea maoni ya uandaaji wa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 wakifuatilia mkutano*

# PPAA wapatiwa mafunzo ya NeST, Moduli ya Rufaa na Malalamiko kwa njia ya kieletroniki kuanza



*Kamishna wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya NeST kwa Wajumbe wa Mamlaka ya Rufani, Menejimenti na Watumishi wa PPAA mjini Iringa. Aliyekaa ukulia ni Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Sauda Mjasiri na upande wake wa kushoto ni Katibu Mtendaji wa PPAA, James Sando.*

**Wajumbe wa Mamlaka ya Rufani,** Uongozi na Watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) wameshiriki mafunzo ya siku tano kuhusu Mfumo wa Ununuzi wa Umma wa Kieletroniki (NeST) Iringa, baada ya kukamilisha moduli ya kupokea na kushughulikia rufaa na malalamiko kwa njia ya kieletroniki.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Kamishna wa Sera ya Ununuzi ya Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga, alisema Serikali inafanya kazi kuhakikisha kuwa moduli tofauti zitapatikana pole pole kwenye mfumo wa NeST, ikiwa imeanza na baadhi ambazo ni muhimu na mafanikio makubwa tayari yanajitokeza, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa uwazi, uwajibikaji, na ushindani wa haki.

“Kwa sasa, Serikali inaweza kupata moja kwa moja taarifa kuhusu shughuli za manunuzi ya taasisi, kama vile idadi ya zabuni zilizoshughulikiwa, thamani yake, mikataba iliyotolewa hadi sasa, na ni zipi zinaonekana kuwa na masuala yanayohitaji kushughulikiwa,” alisema Dkt. Mwakibinga, akibainisha kuwa mfumo uliopita haukuweza kutoa taarifa kama hizo.

Zaidi ya hayo, alisema kukamilika kwa Moduli hiyo kutaimarisha ufanisi katika mchakato wa Ununuzi ya Umma, kufanya iwe rahisi kutoa haki kwa uwazi kwa kuharakisha kushughulikia malalamiko.

“Kwa kuwa kila kitu kinafanyika kwa uwazi ndani ya NeST, sasa tunaweza kutarajia malalamiko machache kutokea,” aliongeza Dkt. Mwakibinga, huku akitoa tahadhari kwa PPAA kwamba baadhi ya wazabuni wanaweza kukata rufaa kwa maamuzi kwa nia mbaya ya kuchelewesha mchakato, wakijua kuwa wamepoteza kwa haki.

“Ni muhimu kuhakikisha kuwa haki ya kukata rufaa haitumiwi vibaya kuzuia mchakato kwa wazabuni wengine, bila shaka mtu anayetumia haki yake vibaya ya kuzuia mchakato wa zabuni pia anapaswa kukabiliana na matokeo,” alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Sauda Mjasiri, aliishukuru Serikali kwa juhudi zake za kuongeza ufanisi wa mfumo wa ununuzi ya umma na kuingiza katika NeST moduli ya kupokea malalamiko na rufaa za zabuni ■

# HABARIPICHA




*Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Sauda Mjasiri, akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo ya NeST kwa watumishi wa PPAA mjini Iringa*




*Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande (Mb.) akipokea zawadi kutoka kwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani Jaji Mstaafu Mhe. Sauda Mjasiri hivi karibuni baada ya kufungua rasmi mafunzo ya siku mbili Jijini Dar es Salaam kuhusu moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki*




*Mgeni rasmi akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa PPAA wakati wa mafunzo ya siku mbili juu ya moduli ya uwasilishaji wa malalamiko/rufaa kwa njia ya kieletroniki Jijini Dar es Salaam*